**JINA: ………………..……………………………...………NAMBARI: ……….. KIDATO: …………**

**KISWAHILI KIDATO CHA PILI**
**MWISHO WA MUHULA WA TATU**
**MUDA: SAA MBILI NA NUSU**

# THE STANDARD MEASURE SERIES FORM 2 END OF YEAR EXAMS 2023.

**Jibu maswali yote kwenye nafasi zilizoachwa wazi**

**SEHEMU A: INSHA ALAMA 20**
Andika ratiba ya siku ya wazazi shuleni.

------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------

**UFAHAMU (AL 15)**

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.

**ULEVI**

Ilikuwa Jumamosi ya mwisho wa mwezi, wakati wa magharibi, nikiwa kwenye tembea zangu za kupunga hewa. Nikaona kilee, kijitu si kijitu, mtu. Kinakuja kwa kinyume huku na huku kama kwamba kikiendeshwa na upepo.

Kukaribiana nacho, nikaweza kukiona vizuri zaidi. Kilikuwa kirefu, lakini kilichokonda na kukondeana mithili ya kiuno cha nyigu. Shati kiliyovaa ilionekana kama kwamba imetundikwa tu kijitini. Kukikazia macho, nilitambua. Maskini! Mwili wake ulidhoofika na kuwa kitu kama vile mfuko tu wa mifupa. Kufumba na kufumbua, kilianguka bwup! Chini. Nikajikuta nikitikisa kichwa.
“Vipi mlachake bwana we?’’ Nikamtupia, huku nikijaribu nikitikisa kichwa.
“Vi-vi-vipi ni-nini?’ akanirudia.
“Umerudia he ?’’
“La-lakini kwa pe-pesa zangu, si-si-siyo kwa-kwa-kwa kudoea.’’
“Daktari alikushauri vipi ?’’
“A-acha-ch-chana na yeye hu-huyo. Ati nina-naji-jipunguzia maisha. Kwa ni-ni-nani ha-hata-ta-kufa?’’

Kuzidi kumnyanyua ili nimwinue kutoka chini, akanitazama kwa macho yake malegevu na kuniuliza,
“Ha-hata wewe pi auna-na- nataka kuniibia ?’’
“Nani amekuibia?’’ nikamwuliza kwa mshangao. Kimya. Aliweza kuinuka na kubaki akiyumbayumba mfano wa mcheza rumba. Kisha yakamtoka matusi mfululizo.
“Mlachake!’’ Ikanitoka sauti ya mshangao baada ya kushuhudia yale niliyoyatia machoni.

“Ni aibu gani hii ya kujitapikia ovyo?’’
“Ni me-jiji-jitapikia ni-ndiyo. Sikumta-tapikia mtu.’’
“Sikiza Mlachake bwana.’’
“Ndio-ndiyo bwana m-mkubwa,’’ akasema na kunipigia saluti . Kisha, kwa mara nyingine tena, huyoo akasalimu amri.
“Mlachake ! Pesa, ulizifanyia, kazi mwezi mzima ili zije kukutesa namna hii he ?’’
“Ndi-ndiyo. Cha m-m-mgema hu-uliwa na mle-levi si-si ndiyo ?’’

Kwa mara nyingine tena, nilijikuta natikisa kichwa. Papo hapo, akili ikanipa kuwa nimsaidie kwa kumfikisha nyumbani kwake.
Kufika mlangoni tu, alipaaza sauti akisema, “Fungua !’’ ilhali mlango ulikuwa umekomewa kutoka nje. Kisha dwa ! Akaupiga teke, halafu “Huuwi !’’ akatisha. Akuchutama na kubwagizika chini mfano wa gunia tupu. Nikatikisa kichwa na kujiendea zangu.

MASWALI

1. Taja sababu mbili za mlachake kuonekana akiyumbayumba. (ala 2)

2. Mbali na kumletea mtu aibu kama vile ya kujitapikia ovyo, taja athari au hasara nyingine tatu za ulevi kwa mlevi. (ala 3)

3. Mwandishi anasema, "Kwa mara nyingine tena huyoo, akasalimu amri.'' Anamaanisha nini hasa kwa kusema "akasalimu amri ?'' (ala 1)

4. Ni aina gani mbili za ushahidi zinazotudokezea kuwa Mlachake hakuishi peke nyumbani kwake ?(ala 2)

5. i) Ni methali gani iliyomjia Mlachake kichwani wakati alipozungumza na msimulizi wa makala haya?(ala 1)

ii) Eleza jinsi methali hiyo inavyoingiliana na maudhui ya makala haya. (ala 2)

6. Eleza matumizi yafuatayo ya lugha kama yanavyojitokeza katika makala uliyosoma. (ala 4)
i) Wakati wa magharibi

ii) Kukutesa

iii) Kudoea

iv) Akili ikanipa

**SEHEMU B: SARUFI (ALAMA 40)**
1. Pambanua sauti hizi kama ni ghuna au si ghuna. (ala 2)
/z/
/k/

2. Eleza maana ya kiimbo. (ala 2)

3. Eleza maana ya shadda. (ala 2)

4. Eleza maana ya mofimu. (ala 2)

5. Andika kwa wingi sentensi hizi. (ala 4)
i) Goti la mtoto liliumia.

ii) Ukwato wa ngamia ni mpana.

6. Bainisha nomino hizi ni za aina gani. (ala 2)
i) Sukari

ii) Mapenzi

7. Tumia vivumishi vya sifa katika mabano kukamilisha sentensi zifuatazo. (ala 2)
i) Mtoto yule ni (nene)

ii) Bei ya meli ni (ghali)

8. Jaza pengo kwa kiulizi sahihi kisha uandike sentensi kwa wingi. (ala 2)
Ni mpishi ……………….. aliyepika ?

9. Fafanua maana ya msemo ufuatao. (ala 2)
Kula mate

10. Andika katika udogo. (ala 4)
i) Jiji hili litapanuka upesi.

ii) Jizee lililokosa adabu limekaripiwa.

11. Geuza sentensi zifuatazo katika hali ya usemi halisi. (ala 4)
i) Reheni alishauriwa na kasisi aache tabia mbaya.

ii) Mwalimu alimwambia Premji afanye bidii katika masomo yake.

12. Andika vitenzi vifuatavyo katika hali ya kutendeshana. (ala 2)
i) Penda

ii) Endesha

13. Tambua kikundi nomino (KN) na kikundi Tenzi (KT) katika sentensi zifuatazo. (ala 2)
Anatembea kwa madaha kama tausi.

14. Kanusha sentensi zifuatazo. (ala 2)
i) Mimi nilicheza

ii) Wewe huchora

15. Kamilisha methali ifuatayo. (ala 1)
Cha kuvunda

16. Andika kunyume cha maneno yafuatayo. (ala 2)
i) Tandika

ii) Umba

17. Pambanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mstari. (ala 4)

Naimba huku nafanya kazi.

**ISIMU JAMII (ALAMA 10)**
i) Eleza sifa za lugha ya hotelini. (ala 10)

FASIHI SIMULIZI (ALAMA 15)

1. Taja na ueleze aina nne za hadithi. (ala 4)

2. Eleza umuhimu wa hadithi. (ala 6)

3. Taja umuhimu wa fomyula za kuanza katika hadithi. (ala 3)

4. Taja umuhimu wa fomyula za kumaliza katika hadithi. (ala 2)

*Contact 0724333200/0795491185 for marking schemes or order online at*
*www.kenyaeducators.co.ke*